MOI HIGH SCHOOL KABARAK

*TRAIL 1 2024*

**Kenya Certificate of Secondary Education**

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**
   **MAJIBU**
   1. Eleza mbinu tano zinazoweza kutumiwa kutatua tatizo **kuu** linalozungumziwa. (al 5)
      i) Kuwaelimisha wakulima kuhusu mbinu bora za ukulima
      ii) Kuwapa wakulima mbegu zitakazohimili kiangazi
      iii) Kuzingatia ukulima wa kunyunyuzia maji
      iv) Uhifadhi mzuri wa mazao
      v) Ardhi itolewe kwa kilimo
      vi) Wakulima waelimishwe kuhusu umuhimu wa kuzuia mmomonyoko wa udongo
      vii) Mazao yanunuliwe kwa bei nafuu
      viii) Sera iwe na sera mwafaka za kukabiliana na tatizo hili la njaa

      (1x5) Hoja za kwanza tano
   2. Fafanua matatizo mbalimbali yanayolikumba Taifa la Kenya. ( al 4)
      i) Tatizo la njaa kwa sababu ya kutegema mvua isiyotabirika
      ii) Tatizo la bidhaa za ukulima kuwa ghali
      iii) Tatizo la vita vya kikabila
      iv) Tatizo la bei duni ya mazao

      (1x4) hoja zozote nne
   3. Onyesha ukulima ulivyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa la Kenya (al 2)

      Ukulima hutegemewa na wananchi wengi kujipatia pato pamoja na chakula. (2x1)
   4. Vita vya kikabila husababisha njaa. Thibitisha kwa mujibu wa kifungu. ( al 2)

      Vita vinapotokea watu huhama na kuacha mashamba.

      Kuchomwa na maghala ya chakula. (1x2)
   5. Eleza maana ya maneno haya kama yaliyotumika katika kifungu. (al 2)

   i) Kukabiliana – Jitihada ya kutatua tatizo fulani
   ii) Janga - maafa/taabu/balaa
2. **UFUPISHO (ALAMA 15)**

   a) Fupisha aya tatu za kwanza. ( maneno 80-85). (alama 9, moja ya mtiririko)

i) Teknolojia haiwezi kuepukika katika malezi ya watoto
ii) Mtandao unaweza kukuza talanta za watoto
iii) Watoto wanafaa kukingwa na hatari za mtandao
iv) Wazazi wanaweza kutumia mitandao kukuza vipawa vya watoto
v) Lazima wazazi wahakikishe usalama wa watoto wao

vi) Watoto waweza kuandika blogu, kujifunza kupiga, kutangaza na kuuza picha na video
vii) Watoto waweza kunoa vipawa katika michezo na kuhimiza ubunifu
viii) Wazazi wanaoruhusu watoto kutumia mtandao kuwapa ufunguo wa ufanisi maishani
ix) Mtandao husaidia mtoto kuweka rekodi ya ufanisi wake
x) Rekodi hizi huwatia moyo kukuza talanta zinazoweza kuwafaa katika maisha ya baadaye.

b) Fupisha aya ya nne. (maneno 35-40) (alama 4, moja ya mtiririko)
i) Wazazi wachunguze na kupitisha chochote watoto wanapakia au kuchapisha.
ii) Wafanye hivi ili wasihatarishe maisha yao na familia zao
iii) Wazazi wawe makini ili watoto wasiandike maelezo yanayoeleza wanakoishi
iv) Waepuke kutangaza vitu kama sare za shule, anwani au picha zao.

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a). Andika sauti zanye sifa zifuatazo: (al 2)

i) Kipasuo, si ghuna cha ufizi /**t**/
ii) Kikwamizo, ghuna cha ufizi /**dh**/
iii) Nazali, ghuna ya kaakaagumu /**ny**/
iv) Irabu ya mbele, juu, tandazwa /**i**/

b) Tunga neno lenye sauti mwambatano ya ufizi. **ndwele** (al 1)

c) Kwa kutoa mifano, eleza tofauti ya silabi wazi na funge. (al 2)

**Silabi wazi- silabi wazi huishia kwa irabu. Kwa mfano, ba-ba**

**Silabi funge- silabi funge huishia kwa konsonanti. Kwa mfano. Dak-ta-ri**

d) Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (al 2)

Tukipanda ndizi hizi vyema, vijiji hivi vitakuwa na vyakula vya kutosha.

**Nikipanda ndizi hili vyema, kijiji hiki kitakuwa na chakula cha kutosha**

e) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao (al 2)

KN(W+V) + KT (t+ s)

**Yule hodari ndiye aliyenifunza.**

f) Ainisha viambishi awali na gtamati katika neno lifuatalo. ( al 2)

Ulijuaje

U-li-ju-a-je

U } viambishi awali
li }

ju – mzizi

a } viambishi tamati

je

g) Onyesha na kutoa mifano, miundo miwili ya nomino katika ngeli ya KI-VI. ( al 2)

**ki-vi kwa mfano; kiti-viti**

**ch-vy kwa mfano; chakula - vyakula**

h) Yakinisha sentensi hii katika nafasi ya pili. ( al 2)

Wasiposoma kwa bidii hawatapita mtihani.

**Ukisoma kwa bidii utapita mtihani**

i) Akifisha sentensi ifuatayo. (al 2)

tafadhali nipe maji ninywe nina kiu mkimbizi alimwambia

**"Tafadhali nipe maji ninywe. Nina kiu." Mkimbizi alimwambia.**

j) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo umoja. ( al 1)

Ngoma hizo zao zilipasuliwa na vijana wale.

**Kigoma hicho chake kilipasuliwa na kijijana kile.**

k) Tunga sentensi **moja** ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendua. ( al 2)

Funga

Chomeka

Jibu: Mama **alifungua** mlango na **kuchomoa** ufunguo.

(kadiria sentensi ya mwanafunzi)

l) Unda vivumishi kutokana na vitenzi vifuatavyo kisha utunge sentensi ukitumia vivumishi ulivyotunga. ( al 2)

i) **Cheka**
Kivumishi **mcheshi**
Sentensi **Mtoto mcheshi hupendwa na wengi.**

ii) **Pika**
Kivumishi **mpishi**
Sentensi **Mama mpishi amepika chakula kitamu**.

m) Tumia neno **hadi** katika sentensi kama kihusishi cha: (al 2)

i) wakati

ii) mahali

**Wanafunzi walifunga safari ya Nairobi hadi Mombasa kutoka asubuhi hadi jioni.**

n) Tambua aina za vielezi katika sentensi ifuatayo: (al 2)

Kipusa mrembo sana alitembea kitausi shuleni jana.

**Sana - kielezi cha namna halisi**

**Kitausi – kielezi cha namna mfanano**

**Shuleni – kielezi cha mahali**

**Jana – kielezi cha wakati**

o) Huba ni kwa penzi, heshima ni kwa **adabu** na ruhusu ni kwa **udhuru** (al 1)

p) Tambua aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Kijana aliyekuwa hapa ndiye mtoto wake.

**Aliyekuwa – kitenzi kishirikishi kikamilifu**

**Ndiye – kitenzi kishirikishi kipungufu**

q) Tambua shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. (al 3)

Vijana hawa hulipiwa karo mapema.

**Shamirisho kipozi –** **karo**

**Shamirisho kitondo –** **vijana hawa**

**Chagizo -** **mapema**

r) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali. (al 2)

Zawadi nzuri niliyomtunuku mwanawe ilimpa furaha tele.

| S (changamano) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| KN | | | KT | | |
| N | V | s | T | N | V |
| Zawadi | nzuri | niliyomtunuku mwanawe | Ilimpa | furaha | tele |

s) Tunga sentensi mbili ukitumia neno "komaa" kama: (al 2)

Kivumishi - **mkomavu**

**Mtu mkomavu hutoa maarifa**

Nomino – **ukomavu**

**Ukomavu wake uliwasaidia watu sana**

t) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo; (al 3)

Ndovu amelala kando ya mti.

**Ndovu -** **kirai nomino**

**Amelala -** **kirai tenzi**

**Kando ya mti -** **kirai husishi**

u) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana tofauti za maneno; **Fuma** (al 1)

fuma- unda kitambaa kwa kupitisha nyuzi ndefu juu na chini kwa kutumia sindano

fuma- piga kwa kumrushia mtu mkuki au mshale

fuma – ona mtu ghafla akifanya jambo fulani

**sentensi; Alimfuma mnyama yule kwa mshale alipofumania akila mimea shambani.**

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**majibu**

a) Tambua sajili inayorejelewa katika kifungu hiki. (alama 1)

**Sajili ya shuleni/ darasani**

b) Fafanua sifa nne za sajili hii kama zilivyojitokeza katika kifungu ( alama 4)

Msamiati maalum mfano, mwalimu, kitabu

Lugha rasmi

Lugha ya utani na ucheshi baina ya wanafunzi

Lugha sanifu

Kubadili msimbo

Lugha ya kudadisi (mwanafunzi atoe mifano kutoka kwa kifungu)

i) Taja nadharia tatu zinazoeleza chimbuko la lugha ya Kiswahili. ( alama 3)

1. **Kiswahili ni lugha ya mseto**
   Kwamba Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha za waarabu, wahindi, waajemi na wenyeji wa pwani.

2. **Kiswahili ni kiarabu**
   Kwamba msamiati wa kiarabu ndio unapatikana katika lugha ya Kiswahili, hivyo basi Kiswahili ni kiarabu.

3. **Kiswahili ni mojawapo wa lugha za kibantu**

Kwamba kuna ushahidi wa kiisimu na kihistoria. Msamiati kubwa unaopatikana katika lugha ya Kiswahili una asili ya kibantu.

ii) Eleza istilahi zifuatazo katika isimu jamii (alama 2)

a) Usanifishaji

Ni uamuzi wa kuchagua lugha moja au mojawapo wa lahaja za lugha ili kuifanayia marekebisho ya kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi ili itumike katika shughuli rasmi.

b) Lafudhi

Ni ule upekee wa mzungumzaji katika lugha.